***TALKING NOTES* ZA MHE. THOBIAS E. M. ANDENGENYE, MKUU WA MKOA WA KIGOMA WAKATI AKIZUNGUMZA NA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI**

TAREHE 03 JUNI, 2021

UTANGULIZI

Mhe. Baraka Naibuha Lupoli - Mstahiki Meya wa Manispaa,

Mhe. Samson Rainald Anga - Mkuu wa Wilaya,

Mhe. Mgeni Omari Kakolwa - Naibu Meya wa Manispaa,

Ndg. Ferdinand Filimbi - Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa,

Ndg. Valence Rutakyamirwa - Mkaguzi Mkuu wa Nje (NAOT),

Ndg. Yassin Mtalikwa - Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya,

Ndg. Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ndg. Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Wilaya,

Wah. Madiwani,

Ndg. Watendaji katika ngazi mbalimbali,

Ndg. Wageni Waalikwa,

Ndg. Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mstahiki Meya,

- Natoa Shukrani kwa Uongozi wa Wilaya ya Kigoma na Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji kwa Mwaliko wa kushiriki na kuzungumza na Wajumbe wa Baraza la Madiwani na Wananchi waliofika kufuatilia Mkutano huu Maalum wa kujadili **Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020**.

- Hii ni mara yangu ya kwanza kupata nafasi ya kuzungumza nanyi katika Baraza lenu tangu nilipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

- Hili ni jambo la heshima kwangu na litanipa fursa ya kusikiliza namna mnavyoendesha majadiliano yenu na kuwashauri kadri itakavyohitajika.

- Nawapongeza kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu licha ya changamoto kadhaa mnazokabiliana nazo.

- Nawashukuru nyote kwa mahudhurio yenu mazuri.

TAARIFA YA CAG KWA HESABU ZA MWAKA 2019/2020

Mstahiki Meya,

- Nimesoma Ripoti Kuu ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo pamoja na mambo mengine imeonesha kuwa Halmashauri yenu ni miongoni mwa

Halmashauri 53 nchini zilizopata **Hati yenye Shaka** (sawa na asilimia 29) kati ya Halmashauri 185 zilizokaguliwa.

- Kwa Mkoa wa Kigoma, Halmashauri yenu ni miongoni mwa Halmashauri sita zilizopata hati yenye shaka ikiwa imeungana na; Halmashauri ya Mji Kasulu, Halmashauri ya Wilaya Buhigwe, Halmashauri ya Wilaya Kakonko, Halmashauri ya Wilaya Kasulu na Halmashauri ya Wilaya Uvinza

- Kama mnavyofahamu, Halmashauri mbili katika Mkoa wetu zilipata **Hati Zinazoridhisha** (zikiwa miongoni mwa Halmashauri 124 zilizopata Hati hiyo nchini). Halmashauri hizo ni; Halmashauri ya Wilaya Kigoma na Halmashauri ya Wilaya Kibondo.

- Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibainisha hoja 4 zifuatazo kuwa ndiyo msingi wa hati yenye shaka aliyotoa;

a. Maelezo yasiyojitosheleza kuhusiana na madai yaliyopoteza thamani Sh. 320,106,707

Maelezo Na. 20 kwenye taarifa za fedha yameonesha kupungua kwa thamani ya madai kwa Sh. 320,106,707 kulikotokana na mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki (hayakupokelewa na Halmashauri), lakini hakukuwa na maelezo kuhusiana na chimbuko la kupungua kwa madai hayo, mikakati ya menejimenti na hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha kiasi hicho cha madai kinakusanywa.

b. Mapato yatokanayo na huduma ya maegesho ya pikipiki ambayo hayakupokelewa Sh. 105,780,900

Mkaguzi alibaini kuwa, Halmashauri ilitoa stika zenye namba maalumu kwa wamiliki wa pikipiki, ambapo kiasi cha Sh. 172,848,000 kilitakiwa kiwe kimekusanywa kama mapato ya ada ya maegesho ya pikipiki; lakini ni kiasi cha Sh. 67,067,100 tu ndicho kilithibitishwa kupokelewa benki wakati kiasi cha Sh. 105,780,900 hakikuonekana benki na wala hakikutambuliwa kwenye taarifa za fedha.

c. Kushindwa kujiridhisha na marekebisho ya hati za madai Sh. 31,301,318

Mkaguzi alibaini kuwa, marekebisho ya hati za madai ya mapato ya Sh. 31,301,318 yaliidhinishwa kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) na afisa ambaye hakuwa na mamlaka ya kuidhinisha marekebisho hayo. Pia, alibaini kuwa marekebisho hayo yalianzishwa na afisa wa Halmashauri bila ya kuwepo kwa maombi ya kufanya marekebisho hayo kutoka kwa wakusanya mapato.

d. Malipo yasiyokuwa na nyaraka toshelezi Sh. 20,953,230

Halmashauri ilifanya malipo ya Sh. 20,953,230 kwa walipwaji mbalimbali ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi, hivyo Mkaguzi alishindwa kujiridhisha na usahihi na uhalali wa malipo hayo.

- **Ninawashauri mjibu Hoja zote zilizowasababishia Hati Yenye Shaka zilizobakia ili zifungwe kabla ya Ukaguzi ujao. Aidha, hakikisheni mnaepukana na hoja za aina hiyo wakati mwingine.**

- Pamoja na hoja hizo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebainisha mapungufu mengine kwenye hesabu zenu ikiwemo;

    - Halmashauri iliwasilisha kitabu cha hesabu za mwisho kilichokuwa na mapungufu mbalimbali ambayo yalipelekea kupungua au kuongezeka kwa baadhi ya vipengele vya taarifa hiyo. *Nawashauri mkamilishe kitabu cha hesabu zenu mapema ili kutoa fursa kwa Menejimenti kukipitia na kufanya maboresho iwapo yatahitajika kabla ya kuwasilishwa kwa Mkaguzi.*

    - Halmashauri haikupeleka sh. 80,864,967 sawa na asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenye vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. *Nashauri fedha hizo zipelekwe na Mkaguzi apewe nyaraka ili afanye uhakiki.*

    - Halmashauri ilifanya Manunuzi yenye thamani ya sh. 7,182,120 bila ushindani wa bei. *Nawasisitiza kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na Kanuni zake na kuepuka makosa ya aina hiyo.*

- Hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka ya nyuma inaonesha kwamba

mapendekezo **52** yalitolewa kwa Halmashauri yenu ambapo mapendekezo **4** yametekelezwa, mapendekezo **33** yako katika hatua ya utekelezaji na mapendekezo **15** hayajatekelezwa. *Nashauri mjiwekee mkakati madhubuti wa kutekeleza mapendekezo yote ya miaka ya nyuma.*

- Kwa upande wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) hali halisi ya utekelezaji kwa miaka ya nyuma inaonesha kwamba maagizo **6** yalitolewa kwa Halmashauri yenu ambapo, agizo **1** limetekelezwa na maagizo **5** yanaendelea kutekelezwa. *Kasi hii ya utekelezaji hairidhishi. Nashauri mjiwekee mkakati madhubuti wa kutekeleza maagizo yote ya LAAC ya miaka ya nyuma.*

MAELEKEZO YA NYONGEZA KUHUSU TAARIFA YA CAG

Mstahiki Meya,

- Katika mkutano wa leo mnalo pia jukumu la kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria Watumishi waliobainika kuhusika na vitendo vya ubadhirifu (kama wapo) na kutowajibika ipasavyo na hivyo kuiletea Halmashauri yenu hasara au hoja ambazo katika hali ya kawaida ya utendaji makini zisingepaswa kutokea. Uchukuaji huu wa hatua ulenge Watumishi wote waliohusika katika ngazi zote (ngazi za chini, kati na Makao Makuu ya Halmashauri).

- Imarisheni uwajibikaji kwenye usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine, zingatieni taratibu za fedha na imarisheni mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuepuka kupata Hati Isiyoridhisha.

- Hakikisheni hoja za ukaguzi zinajibiwa mapema na majibu kuwasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Nje ili afanye uhakiki. Msirundike hoja, zitawashinda kujibu.

- Halmashauri itenge Bajeti ya kutosha ili kuweza kuwapeleka Wahasibu na Wakaguzi kwenye Mafunzo ya mara kwa mara yanayoendeshwa na wataalamu wa Ufungaji wa Hesabu ili kuweza kupata miongozo mipya na marekebisho yake (IPSAS).

- Halmashauri itoe kipaumbele katika maandalizi ya Hesabu za Mwisho kwa kuhakikisha waandaaji wanawekewa mazingira mazuri wakati wa zoezi hilo na kuwaondolea mwingiliano kati ya jukumu hilo na majukumu yao mengine ya kila siku.

- Afisa Masuuli ahakikishe unakuwepo uhusiano mzuri/ushirikiano kati ya Menejimenti za Halmashauri na Wakaguzi wa Nje na wahakikishe nyaraka zote zinazohitajika zinapatikana kwa wakati.

- Menejimenti ya Halmashauri ihakikishe Taarifa ya Fedha inaandaliwa kwa usahihi na kuzingatia miongozo na viwango vinavyoelekezwa.

MASUALA YA KUZINGATIA

Mstahiki Meya,

Masuala yafuatayo yazingatiwe:

i. Zingatieni Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utekelezaji wa Majukumu yenu. Katika eneo hili mnaongozwa na Kanuni za Maadili ya Madiwani na Kanuni za Maadili kwa Watumishi wa Umma. Ni utovu wa Maadili na ni uvunjaji wa Sheria kwa Wah. Madiwani na Watumishi wa Umma kutumia nafasi na Madaraka yao kujipatia Mikataba na Zabuni mbalimbali ni makosa pia kwa Viongozi na Watendaji kutumia vibaya fedha na mali nyingine za Serikali.

ii. Simamieni ubora na viwango katika Miradi inayotekelezwa kwenye Kata zenu. Nawashauri muwakemee Watendaji wasiozingatia ubora katika usimamizi wa Miradi inayotekelezwa na pale inapobidi Mamlaka zishauriwe kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma.

iii. Fanyeni tathmini ya kina ya uwezo wa vyanzo vyenu vya mapato na wekeni mikakati inayotekelezeka ya kuongeza ukusanyaji wa mapato. Kwa mujibu wa taarifa zenu za mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri yenu ilikusanya mapato pungufu kwa asilimia **39** ya lengo la mwaka. Kutokana na hali hiyo, Halmashauri yenu ilikuwa na uwezo wa

kujitegemea wa **asilimia 7** tu. *Hakikisheni mnatumia vyema Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato.*

iv. Simamieni na hakikisheni fedha kwa ajili ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu zinatengwa na kutolewa kwa walengwa. Fedha hizi ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri (yasiyo ya masharti). Fikirieni kutoa Elimu na ushauri sahihi kwa walengwa kabla ya kuwapa mikopo hiyo. ***Mnakumbushwa pia kufuatilia marejesho ya mikopo iliyotolewa katika miaka ya nyuma***.

v. Afisa Masuuli wa Manispaa ahakikishe Wakuu wa Idara na Vitengo wote wanahusika katika utoaji wa taarifa muhimu kwa ajili ya kuandaa taarifa ya fedha. Afisa Masuuli anapaswa kuhakikisha ubora na usahihi wa taarifa zinazowasilishwa kwa ukaguzi.

HITIMISHO

Mstahiki Meya,

Kwa kuhitimisha;

- Natoa msisitizo kwamba Halmashauri iimarishe usimamizi wa vyanzo vya mapato na ufuatiliaji wa makusanyo. *Kuweni wabunifu na ibueni vyanzo vipya vya mapato*.

- Boresheni utoaji huduma na tatueni kero za Wananchi kwa wakati.

- Zibeni mianya yote ya upotevu wa mapato. Manispaa inapoteza mapato mengi kutokana na udhaifu mkubwa wa baadhi ya Watendaji na mifumo ya ukusanyaji isiyosimamiwa vizuri.

- Wekeni utaratibu mzuri wa uondoshaji taka mitaani. Kuna baadhi ya Maeneo taka zimeachwa zimerundikana kwa muda mrefu bila kuondolewa. Katika baadhi ya mitaa kuna wananchi wanaendelea kuchimba mashimo kwa ajili ya kutupia taka. **Huu si utamaduni wa Mjini. Naelekeza tuachane na utamaduni huo**.

Akhsanteni kwa Kunisikiliza.